

kushauriwa na kupimwa kwa kujitolea virusi vya ukimwi(VCT)

Kushauriwa na kupimwa kwa kujitolea (VCT) inamaanisha nini?

Kupimwa ugonjwa wa ukimwi unianza wakati mtu anaambukizwa virusi vya ukimwi na bado hajapata ugonjwa wa ukimwi .VCT ni njia mpya ya kupima virusi vya ukimwi na pande nyingi duniani hutumia njia hii na mpaka sasa wamefanikiwa.

kupimwa kwa kujitolea inamaanisha nini?

Hii inamaanisha yakwamba ni wewe umejitolea kupimwa na hauja lazimishwa na mtu yeyote.Mtu yeyote ambaye anataka kupimwa hushauriwa na mshauri ili aweza kuamua kama anataka kupimwa au la. Unaweza kukataa kupimwa wakati wowote.

Kwanini nafaiwa kushauriwa kabla ya kupimwa?

Ili kuhakikisha yakwamba umeelewa sababu ya kupimwa ,njia inayo tumika kupimwa na matokeo.Pia ili uweze kumuuliza mshauri maswali yeyote kuhusu ugonjwa huu. Ukikubali kupimwa baada ya kushauriwa unafaiwa kujaza fomu ya kukubali na kuweka saine.

Njia ya kupimwa?

Mara tu virusi vya ukimwi hui ingia mwilini protini inayoitwa antibody hujulisha kinga cha mwili. Wakati wa kupimwa vipimo hutafuta hiza antibody ili kuonyesha kama mwili una virusi vya ukimwi , teknolojia mpya imesaidia na matokea huonyeshwa baada ya dakika thelathini.

Ni nini hufanyika wakati wa kupimwa?

Kipimo hufanywa na muuguzi ama mtu ambaye amefundishwa kupima . Kwanza unatolewa damu kutoka kwenye kidole ama mkono halafu unangojea matokeo. Matokea yanaweza kurudiwa na ita bidi upeane damu tena.

kipimo hiki ni kamili?

Kipimo cha antibody huwa na ukamili wa asilimia tisaini na tisa na nukta tano (99.5%)

kipimo hiki kinaweza fanywa mara mbili au tatu ili kuhakikisha.

Kuna mara nyingine ambapo kipimo kinaweza kurudiwa kama vile:

- ume ambukzwa ugonjwa hivi karibuni (kawaida kati ya wiki tatu hadi miezi tatu) na mwili bado haijaanza kutengeneza protini ya antibody.
- watoto wadogo ambao wamezalia na wamama wenye virusi vya ukimwi na bado wako na protini ya antibody ya mama zao mwilini na kwa hivyo wakipimwa matokeo yataonyesha virusi.

matokeo yanamaanisha nini?

matokeo halisi yanamaanisha mwili una virusi vya ukimwi.

Na matokeo ambayo si halisi inamaanisha mwili hauna virusi vya ukimwi.

Nani ataelezewa matokeo ya kipimo?

Matokeo ni ya siri nani wewe tu unaweza eleza mtu unayotaka.

Ni nini hufanyika baada ya mashauri ya mwisho?

Baada ya kupata matokeo , mshauri ata kuongeleza juu ya matokeo.Mshauri atakueleza njia ya kuishi na kukubali matokeo kama utapatikana na virusi na pia nji ya kujikinga kama vile kufanya mapenzi kwa kujikinga kila wakati kama uko na virusi au la.

Matokeo halisi yanamaanisha nini kwangu?

Kama uko na virusi vya ukimwi kuna njia mingi ya kuwa na afya njema na pia ni vizuri kuanza kumeza madawa.Virusi vya ukimwi pia huleta magonjwa kama kifua kikuu na ugonjwa huu unaweza tibiwa.Mshauri wako atakueleza yote unayofaiwa kujua. Pia kuna magonjwa ya zinaa ambayo huendanisha na virusi vya ukimwi na pia yanafaa kutibiwa pia ni vizuri kueleza wapenzi wako ili pia nao wapimwe na kushauriwa.Kama uko mja mzito ni vizuri kumwona daktari na pia kuenda kliniki spesheli ya wamama ili kuzuia kupitishia virusi kwa mtoto.

Matokeo isiyo halisi inamaanisha nini kwangu?

Kama matokea yamehakikishwa sihalisi basi unafaiwa kujikinga na kuenda hospitali mara kwa mara ili kupimwa hali yako , pia kujikinga kila wakati unapofanya mapenzi kwa kutumia kondomu.

Naweza fanya nini ili kujichunga na virusi vya ukimwi?

Kwanza ni kwa kujichunga wakati wa kufanya mapenzi kwa kutumia kondomu , kupanga uzazi, kuenda hospitali mara kwa mara ili kujichunga kutopata magonjwa ya zinaa.

Mshauri wako atakueleza kliniki zilizoko karibu ambazo zinaweza kukusaidia.

Nafaiwa kuwa na kikundi cha kunisaidia?

Vile matokeo yataokea, ni vizuri kuwa na watu wa kukusaidia na kukushauri, Mashauri kuhusu watoto ,nyumba, pesa, maisha ya mbele .mashuri haya ni baada ya kupimwa na ni ya siri lakini unaweza kuja na mtu unayetaka kama vile familia ,mpenzi au rafiki .

Nani anafaiwa kupimwa?

Wanoa himizwa kupimwa ni :

- Mtu yeyote anaye shukiwa kuwa na virusi vya ukimwi
- kama uko na ugonjwa wowote wa zinaa
- kama uko mja mzito
- Umetumia sindano ambayo ime tumiwa na zaidi ya mtu mmoja
- Mfanyi kazi wa hospitali ambaye ameguza damu na ako na kidonda
- kama hauna hakika juu ya tabia za mpenzi wako
- kama unataka kujua hali yako ya ukimwi.